MANYAM FRANCHISE
Discover!Learn!Apply

## 4.2 SEHEMU YA PILI – INSHA

Katika mwaka wa **2015 mada** ya insha ilikuwa:

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.

Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:

Hakika nilikuja kuamini kwamba mtu akitia bidii katika jambo, hata liwe gumu vipi, hatimaye hufaulu.

Swali hili lilitahini uandishi wa insha bunilizi za mdokezo. Mtahiniwa alihitajika kubuni utungo ambao unaonyesha umuhimu wa kutia bidii na kutokata tamaa maishani

**a) Maudhui/yaliyomo**

Hapa mtahiniwa alihitajika kuandika kisa ambacho kilionyesha tukio/matukio magumu ambayo yalimkabili mhusika, mhusika akakabiliana na jambo hilo kwa bidii na mwishowe akafaulu. Anaweza, pia kusawiri mhusika ambaye alikata tamaa , au alikosa kutia bidii na mwishowe akahasirika.
Yafuatayo yaliweza kujitokeza:

i) Mwanafunzi kutoka familia maskini akose karo na mahitaji ya kimsingi, asikate tamaa, apate mfadhili na hatimaye kufanikiwa.
ii) Masomo yawe magumu kwa mwanafunzi, ajibidiishe na hatimaye kuibuka mshindi, n.k.

**b) Muundo na mtindo**

Muundo wa insha ya masimulizi ulihitajika kuzingatiwa. Yafuatayo yalitarajiwa kubainika:

**i)** **Mwanzo** – Mwanzo wa kisa ubainike.Anaweza kuanza kwa mbinu rejeshi.
**ii)** **Mwili** –Hapa ndipo mtahiniwa anapokikuza kisa chake. Matukio mbalimbali yajitokeze. Tukio moja pia linaweza kukuzwa kwa kina.
- Mtindo wa usimulizi ujitokeze.Uteuzi mwafaka wa tamathali za usemi na mbinu nyingine za kimtindo kama vile dayolojia za wahusika, ambazo zinalenga kukuza mada husika uzingatiwe.
- Kaida za kisarufi zizingatiwe.
- Maendelezo mwafaka ya maneno yazingatiwe.
- Insha iandikwe kwa hati nadhifu inayosomeka.

**iii)** **Hitimisho-** Hapa ndipo msimulizi anapohitimisha hadithi yake.Atumie kauli aliyopewa kwa kuioanisha vyema na kisa chake.

### 4.2.1 Vigezo vya kutathminia

Yafuatayo ni maelezo yanayoonyesha jinsi watahiniwa wanavyotengwa katika viwango/vitengo vinne maalum, na mambo ambayo yanazingatiwa ili kumtuza mtahiniwa kiasi fulani cha alama katika vitengo hivi vinne. Vifuatavyo ndivyo vitengo (makundi) vya alama:

(i) 01 – 10
(ii) 11 – 20
(iii) 21 – 30
(iv) 31 – 40

### 4.2.2 Kundi la kwanza (alama 01 – 10)

Watahiniwa katika kitengo hiki hawamudu kujieleza katika Kiswahili. Watahiniwa wanaopata alama **01-05** hasa huwa na mtindo hafifu sana wa kujieleza. Insha zao hukosa muwala na muumano wa mawazo. Baadhi hujieleza kwa kuchanganya maneno ya Kiswahili, Kiingereza na hata lugha zao za mama. Wengine hutumia maneno yasiyoeleweka kabisa. Msamiati hutumiwa kiholela bila uwiano wowote, ama na misamiati jirani, au na mada husika. Udhaifu wao kimawasiliano huwakosesha kuikuza mada/ maudhui ya swali walilopewa.

Watahiniwa wanaotuzwa alama **06-10** hudiriki kujieleza kwa Kiswahili, japo kwa mtindo hafifu. Hata hivyo, insha zao huwa na mategu mengi ya sarufi na hijai ambayo huufifilisha usimulizi/kujieleza kwao. Hawa pia huwa wamepotoka au kupungukiwa kimaudhui/upande wa mada na wengi huhamisha sheria za lugha zao za mama hadi Kiswahili (huwa na athari nyingi za lugha ya mama).

**Mtungo wa kwanza**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:

Hakika nilikuja kuamini kwamba mtu akitia bidii katika jambo, hata liwe gumu vipi, hatimaye hufaulu.

Hakika siku nilikuja kuamini kwamba watu
wakitia bidii katika jambo, hata liwe gumu vipi
hatimaye hufaulu kuwa na ngari mama wangu
nilikuja katika nyumba yangu nikiwa
matifiki wangu. Nilikuwa baba, mutinda pia sei
nyumba yangu ilikuwa na tedio kwamba
watu hufaulu katika kuamini jambo liwe
gumu vipi.

Siku ya moja nilikujo kwa nyumba yangu jambo
nikiwa na rafiki wangu katika mbama yetu
vipi zilikuwa nyingi babu hatimaye watu
hufaulu nilikuja Nilikuwa ngali liwe kuamini
gumu. Zilikuwa dada wetu pia babu yangu nikiwa
jambo kuwa mali nyingi nilikuja katika
shule ya bili.

Siku ya bili nilipata watu kwa nyumba yangu kuamini jambo nusu hakika hafaulu. Tiwe katika mtu yowote bidii ya mtu nilikuja gumu shule ya bili rafiki ngati nusu wiki asa mmaja na nusu nyumba kwa baba yangu nikiwa baba wangu mtu asikiwa kuamini hakika mali yeyote jambo mitindo pia niwika nilipata.

Katika siku ya tatu nilipofika kwa mama wangu ilikuwa na wezi nyumba nilipofika katika kijiji kimeja gumu jambo jana vipi nilikuwa kwa kuamini nilikuja nyumba nikiwa baba mama mali yetu hatimaye hufaulu katika wangu pia baba.

Kijiji cha maana zana gumu jambo la baba Nilikuwa ilikuwa na nikiwa baba. nilipofika hufaulu hatimaye baba kuwa katika kimoja tatu katika kijiji kwa nyinyi zana Jana machakos ilikuwa wezi mama mali kutana jambo. nilipofika tiba zaidi ya Mwanafunzi mwalili mlima shule ya kwaza tena pia kwa zana gumu vipi hufaulu katika wangu maama. Hakika nilikuja kuamini kwamba mtu akitia bidii katika jambo, hata liwe gumu vipi hatimaye hufaulu.

Mtahiniwa huyu hajalenga kiini cha swali. Ingawa ameandika kwa lugha ya Kiswahili, anayosema hayaelekei kuhusiana moja kwa moja na mada. Uakifishaji wa kazi hii ni hafifu mno. Insha imekosa muwala na muumano wa mawazo.

Alama iliyotuzwa: **02**

**Mtungo wa Pili**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:

Hakika nilikuja kuamini kwamba mtu akitia bidii katika jambo, hata liwe gumu vipi, hatimaye hufaulu

Katika kijiji cha Kwato kulikuwa na kijana mmoja asiye penda masomo. Huyo kijana alikataa masomo yake akisema kuwa hawezani na masomo haya. Nanye babu mmoja katika kijiji alimwadithiya kuhusu maisha ya leo ntofauti na ya jana. Huyo babu alikuwa akizema, kuwa, "ziku hizi masomo imekuwa hatari kucheza nayo nikama kucheza na kifo." Kanakwaba kuwa masomo ni chanzo cha maisho.

Huyo babu halimwadithiya kijana huyo bodi akasema hataludi shule. Walimu walimkaza bidii lakini wapi? Huyo kijana haelewi. Katika biblia husema kila mtu ana waza tofauti na la mwingine. Huyo kijana alijikaza kimwanajeshi na kuwa akipita masomo yake.

Wakati alifikiaya mtihani wa shule ya msingi alipita huyo mtihani na kwenda shule ya pili. Huyo kijana alikuwa na furaha kubwa sana kwa mungu kupata na kuweza kusoma. Hata katika msikiti hakuwa hakienda kumsifu mungu lakini sasa hufurahi kwa kuwa babu yake alimshaidia hakuwa bigwa wa taifa

Hata katika michezo alishiriki na mchezo wa kandanda sasa wanacheza Mjina ufaransa kushindana katika mchezo huo wa kandanda za alikuwa akisema kuwa yeye asingemsikiliza babu yake na kumwomba mungu kumshindiye hangekuwa katika hizo nchi za ufraka hapo naipo alikiamini kuwa hakika kwamba mtu akitia bidii ya mchwo katika jambo, hata liwe gumu vipi, hatimaye hufaulu

Mtahiniwa huyu ameielewa mada na kujaribu kuikuza kwa lugha inayoeleweka zaidi. Ingawa insha hii ni bora kuliko ya awali, mtindo wake wa kujieleza bado ni hafifu mno. Mvuto wa insha yake umetingwa na makosa mengi ya sarufi na hijai, Mathalani.

a) **Asiye penda** badala ya **asiyependa**
b) **Hawezani na masomo** badala ya **hayawezi masomo/masomo yamemshinda**
c) **Nanye** badala ya **naye**
d) **ziku** badala ya **siku**
e) **Huyo mtihani** badala ya **huo mtihani/ mtihani huo**
f) **Kupaliki** badala ya **kubariki**

Uakifishaji wake mbaya mno unaishia kuvuruga muwala wa utungo wake.

Alama iliyotuzwa: **06**

**Kundi la Pili (alama 11 – 20)**

Kundi hili huwa na watahiniwa ambao wanaimudu lugha kiasi. Wanaweza kujieleza au kusimulia kwa sentensi au kauli zinazoleta maana. Wale wanaotuzwa alama **11 - 15** huwa na makosa mengi ya sarufi na hijai, na insha zao hukosa mtiririko mzuri wa mawazo.Wengi huwa bado na athari za lugha za kwanza/ lugha za mama.

Wanaotuzwa alama **16 - 20** huwa wameimudu mada kiasi na mtindo wao wa uwasilishaji huwa bora zaidi, ingawa bado huwa chini ya wastani. Wanaweza kutumia msamiati wa kuvutia hapa na pale japo kwa kawaida wengi huutumia msamiati wenyewe vibaya. Insha zao kwa kawaida hutosheleza urefu.

## Mtungo wa Tatu

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:

Hakika nilikuja kuamini kwamba mtu akitia bidii katika jambo, hata liwe gumu vipi, hatimaye hufaulu.

Ilikuwa siku ya Jumatatu ambapo niliamka asubuhi na mapema kabla ya jua kuchomoza miale yake. Nilienda jikoni ambako nilitayarisha kiamsha kinywa. Baada ya kumaliza nilienda moja kwa moja hadi sebuleni na nikaandika meza kwanza tuliombea kicho chakula alafu tukala pamoja. Tulipomaliza wavyele wangu walienda kazini nao ndugu zangu wakaenda shuleni. Nilimbaki nyumbani pekee yangu. Nilikuwa nimehitimu masomo yangu ya darasa la nane, nanilikuwa nimesha uandika mtihani wangu. Nilikuwa nimengojea matokeo ya mtihani huo.

Nilichukua redio nanikaketi chumbani huku nime-ngojea matokeo yangu. Nilimsikia waziri wa masomo akiyatangaza huku akiwa na furaha si haba. Alianza na kusema kuwa wakati huu wanafunzi wamejitahidi katika masomo yao si kama mwaka uliyopita. Kwanza niliJawa na furaha kiasi, lakini moyo wangu ulikuwa unandu danduda huku unga ukiniandama.

Alimeza mate nakutangaza matokeo. Mwanagenzi wa kwanza ni Ruth macharia nilimaka na kudua. Nilipanua mdomo nakana kwamba inzi inaeingia ndani naianze kucheza ngoma. Nilipiga magoti nakumshukuru Mola kwa wema wake mkubwa. Singeweza kuficha furaha yangu niliwafahamisha wavyele wangu. Walifurahi sana midhili ya kibogoyo aliyeota magego na sego au yakutafuna

ubwabwa

Matokeo yangu yalikuwa ifuatavyo.

Hisabati 92%

Kingereza 80%

Kiswahili 90%

Sayansi 98%

Somo ya jamii - 62%

Somo ya dini - 60%

Baada ya muda kidogo magari yalianza kufika nyumbani. Nilitoka nje kuwakaribisha wageni wale. Walikuwa wameandamana pamoja na wavyele wangu. Magari yalikuwa yakupendeza. Waliingia moja kwa moja hadi dani ya nyumba huku yuso zao zikionyesha furaha tele.

Walikuwa wakuu wa elimu na walimu wa shule ambayo nilikuwa nasomea. Palikuwa na wanahabari walikuwa na kamera. Walinihoji kwa wakati kisha wakaenda zao. Walituachia zawadi mingi pamoja na pesa zakunipeleka shuleni. Niliwashukuru, singeweza kuficha furaha yangu.

Hakika nilikuja kuamini kwamba mtu akitia bidii katika jambo, hata liwe gumu vipi, hatimaye hufaulu.

Mtahiniwa huyu anaonyesha kuielewa mada zaidi ya wale wa awali. Ana ubunifu kiasi. Hata hivyo, hajaikuza mada kikamilifu, kadhalika, utungo wake umejaa makosa ya sarufi na hijai ambayo yanaufanya kuwa hafifu mno. Makosa ya kihijai, kimsamiati , kimuundo na kisarufi yanayojitokeza ni kama vile:

- **a)** **juu** badala ya **jua**
- **b)** **sebureni** badala ya **sebuleni**
- **c)** **nilimbaki** badala ya **nilibaki**
- **d)** **nalikuwa** badala ya **nilikuwa**
- **e)** **alianza na kusoma** badala ya **alianza kwa kusoma**
- **f)** **inzi** badala ya **nzi**
- **g)** **yuso** badala ya **nyuso**
- **h)** **zawadi mingi** badala ya **zawadi nyingi**

Alama iliyotuzwa: **12**

**Mtungo wa Nne**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:

**Hakika nilikuja kuamini kwamba mtu akitia bidii katika jambo, hata liwe gumu vipi, hatimaye hufaulu.**

Hapo zamani za zamani paliishi mzee mmoja ambaye alikuwa maskini kupindukia. Alikuwa na wake karibu sita. Alipata watoto wengi na wake hao. Watu kijiji walikuwa wamemheshimu kabisa. Kama ilivyo kama desturi ya wanakijiji ni kuwa mtu ambaye ana watoto wengi hasa vijana alikuwa ameheshimika kijijini. Alikuwa na vijana kumi.

Siku moja aliamua kwenda kutafuta kazi. Siku ya kwanza alienda kwa tajiri mmoja humo kijiji. Alipofika huko alikokuwa akienda alibisha mlango wa tajiri huyo. Alisikia sauti kutoka ndani "Karibu". Aliufungua mlango huo. Alipoingia humo aliulizwa ni nini anachotaka.

Alimwambia tajiri huyo "ninataka kazi kutoka kwako". Tajiri huyo alimuuliza ama akona ujuzi wa kujimba visima. Alisema la! Sina. Aliambiwa ya kuwa hana bahati yoyote. Aliondoka akiwa na huzuni. Alirudi nyumbani akiwa na huzuni mwingi. Wake wake na watoto walishangaa sana.

Siku ya pili ilipofika alienda kutafuta kazi kwa tajiri mwingine. Alipofika huko alikaribishwa kwa furaha na upendo. Alisema kimoyomoyo ya kuwa amepata kazi.

Yeye na tajiri huyo waliingia ndani ya nyumba. Aliulizwa maswali mengi na alifaulu ila swali moja ambalo lilishinda. Swali hilo ndilo ambalo lilikuwa limebeba mambo yote. Hakufaulu. Alirudi nyumbani tena akiwa na huzuni.

Siku ya tatu ilipofika aliamua kwenda kutafuta kazi nyingine. Alienda kwa tajiri ambaye alikuwa akijulikana kijiji. Alipofika huko alishangaa kuona chumba la kifahari. Alibisha kwenye lango kuu. Aliingia humo na kisha akamwomba Mungu akamsaidie. Alibisha mlango wa tajiri huyo hodi! "kuna mtu humo ndani".

Alisikia sauti kutoka ndani, "kuna mtu karibu ndani" bintiye tajiri alijibu. Aliufungua mlango huo na kisha akaiingia ndani. Alimkuta tajiri huyo akiwa ameketi sembuleni. Aliagiza apewe kazi kwa kuwa yeye alikuwa maskini hohehahe. Aliulizwa maswali mengi sana akiyabita.

Alijawa na furaha tele. Swali la mwisho kabisa lilimkanganya mno. Alifeli mtihani huo na kisha akarudi nyumbani. Aliamua kulima. Alipokuwa akilima aliamua kujimba kisima cha maji. Alipokuwa akijimbu alipata kipande cha jiwe ambacho kilikuwa kikimetameta. Alifurahi sana. Aliendelea kujimbua na kisha akajukuwa mkufu ambao ulikuwa

ukimdamdo.

Aliita familia yake ili kusherehekea. Kutoka siku hiyo niliamini kuwa mkungu a anaweza kugeuzia maisha yako. Watoto wake walienda shuleni kusoma na kisha maisha ya mtu huo iliendelea vizuri bila shinda yoyote. Hakika nilikuja kuamini kwamba mtu akitia bidii katika jambo, hata liwe gumu vipi, hatimaye hufaulu

Mtahiniwa huyu amebainisha kuimarika zaidi.Anaitumia lugha kwa wepesi zaidi akilinganishwa na wa awali. Ameielewa mada na kuiwasilisha kwa mtindo wa kiwango wastani. Hata hivyo, hajaikuza mada ipasavyo. Makosa ya kisarufi na hijai, na kimsamiati ni kama vile:

a) **aliuliza** badala ya **aliulizwa**
b) **kijiji** badala ya **kijijini**
c) **akona** badala ya **ana**
d) **kujimba** badala ya **kuchimba**
e) **Chumba la fahari** badala ya **jumba la fahari**
f) **Sembuleni** badala ya **sebuleni**
g) **Shinda** badala ya **shida**
h) **Mkungu** badala ya **mkufu**

Alama iliyotuzwa: **20**

**Kundi la Tatu (Alama 21 – 30)**

Insha katika kitengo hiki huwa inaeleweka vizuri. Hudhihirisha kiasi fulani cha ukomavu wa mawazo. Huwa na mshikamano na mtiririko mzuri kiasi wa mawazo. Insha zinazotuzwa alama **21-25** huwa na ubunifu wa kima cha wastani.Aghalabu watahiniwa hupoteza alama kupitia makosa ya sarufi na hijai, matumizi mabaya ya tamathali za usemi na uakifishaji mbaya. Hata hivyo,, mtahiniwa huwa ameikuza mada vizuri.

Insha zinazotuzwa alama **26-30** huwa na ukomavu zaidi wa mawazo. Maudhui hushughulikiwa kikamilifu zaidi na huwasilishwa kwa mtindo unaovutia zaidi. Insha katika kijitengo hiki hutosheleza urefu.Hata hivyo, insha hizi bado huwa na makosa kiasi ya sarufi na hijai.

**Mtungo wa Tano**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:

ACHANIKAYE KWENYE MPINI HAFI NJAA.

Hakika nilikuja kuamini ~~kwamba mtu~~ akitia bidii katika jambo, hata liwe gumu vipi, hatimaye hufaulu.

Kama ndoni ninafurahia matunda yangu ya bidii na changamoto mchafukoge. Hata hivyo, ninayakumbuka maisha yangu ya kingani kwa huzuni machozi yakinilengalenga. Nililelewa katika malezi duni zaidi; maskini angekoroa akitufuata maskini. Wavyele wangu walikuwa wakonge waliokuwa na mbele wala nyuma. Kwa kweli, tulipiga mbizi katika bahari ya ufukara. Magonjwa chungunzima yalitufika; si waba, si homa ya matumbo, si surua, si utapiamlo, kweli maisha yetu yakawa yananing'inia uzini.

Aghalabu ndugu yangu mlungizi alilialia kwa uchungu wa maradhi yaliyokuwa yakitupata. Chakula nacho kikawa haba. Hakuna jirani yeyote angethubutu kutupa hata maji angalau kuweka kinywani. Tulilalia mate. Licha ya hayo, wavyele wangu wa dhati waningeweza kunilipia karo angalau nipate manufaa ya elimu. Nilitamani sana ardhi ipasuke inimeze ili kuepuka vikwazo vile vyote lakini wapi. Hizo zilikuwa ndoto zo alinacha.

Wavyele wangu hao, hawakuachwa nyuma. Walingang'ana kukidu ili angalau wapate cha kutusaidia. Hatimaye, niliweza kuenda katika shule ya umma. Wahenga nao hawakukosea waliponena, mvumilivu hula mbivu. Walimu huko walikuwa simba.

Sikukata tamaa kwani ni heri nilipata shule yenyewe kuliko kuishi nyumbani. Kwangu ilikuwa ni sharti mithili ya ibada kuvumilia kwani nilikuwa na ari maalum maishani.

Huko niliweza kutangamana na wengine. Niliweza kujua na kutambua dhahiri shahiri kuwa atangaaye sana na jua hujua. Niliweza pia kushirikiana na wanafunzi wenzangu kutatua mambo fulani shuleni kwani kinga na kinga ndipo moto uwakapo. Aidha, kiganja kimoja hakipigi kofi. Angaa niliweza kupata usaidizi katika masomo yote. Mambo eti ya ufukara, nikayaacha kijiji. Niliujenga mustakabali wangu.

Walimu nao hawakusitasita, wajitahidi sana ili alama zangu ziimarike na zidawi. Nami niliweza kutembea na kusonga nao, kwani nilielewa kinaga ubaga, ukibebwa usilevylevye miguu. Hata kama sikuwa wembe wala moto wa kuotea mbali nilielewa bado kuwa, Mungu hamsahau mja wake. Nilitia fora angalau niweze kupata mhisani ambaye angeyadhamini masomo yangu katika shule ya upili. Yakini, nilikumbuka kuwa jitihada haiondoi kudura. Mola naye akaniyeshea baraka.

Baada ya kufanya mtihani wa kunivukisha daraja hadi sekondari, sikuyaamini maninga yangu. Nilikuwa wa kwanza shuleni na alama za kusifia mno. Nao wafadhili hawakusazwa kunikimbilia. Masomo yangu yalizidi kuimarika hadi nilipopata shahada ya uuguzi.

Kweli, achanikaye kwenye mpini hafi njaa. Hakika nilikuja kuamini kwamba mtu akitia bidii katika jambo, hata liwe gumu vipi, hatimaye hufaulu.

Mtahiniwa huyu amebainisha ukomavu zaidi akilinganishwa na wa awali.Ameielewa mada na kuiwasilisha kwa mtindo mzuri wenye mvuto kiasi. Amebainisha wepesi wa kuitumia lugha kukikuza kisa chake.Anatumia tamathali za usemi mwafaka kama vile, **Nilipiga mbizi katika bahari ya ufukara, si homa ya matumbo si surua**..., **atangaye sana na jua hujua, sikukata tamaa**, n.k.
Imebainika kuwa makosa ya kisarufu, kihijai na kimmundo hayavurugi usimuizi wake. Baadhi ya makosa ni:

**a)** **wakonge** badala ya **wakongwe**
**b)** **wa dhati** badala ya **halisi**
**c)** **ng'ang'ana kukutu** badala ya **shikilia kukutu**
**d)** **chungunzima** badala ya **chungu nzima**
e) Matumizi mabaya ya sitiari**: Walimu walikuwa simba**...
f) Matumizi mabaya ya methali: **Mvumilivu hula mbivu**

Alama iliyotuzwa: **25**

## Mtungo wa Sita

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:

Hakika nilikuja kuamini kwamba mtu akitia bidii katika jambo, hata liwe gumu vipi, hatimaye hufaulu.

MCHANIKAYE KWENYE MPINI HAFI NJAA

Kengele ilipigwa, nasi sote tulitoka darasani mwetu na kusimama gwarideni. Haikuwa kawaida kengele kupigwa siku ya Jumatano kwa hivyo wanafunzi walisikika wakiongea kwa sauti ya chini. Mwalimu Mkuu wa shule yetu, Bwana Simba, alisimama mbele yetu na kumkaribisha mgeni aliyekuwa amekuja kutuongelesha, jina lake lilikuwa Bidii Subira. Tulipiga makofi na kumkaribisha yule mgeni.

Bidii Subira alisimama na kuchukua mikrofoni. Alikuwa mja mrefu kama twiga na mtanashati kweli kweli.

"Hitifaki zote zikizingatiwa Hamjambo? Jina langu ni Bidii Subira na nasimama mbele yenu kuwahotubia kuwa ukiwa na bidii utafaulu maishani. Naomba masikio yenu dakika chache tu.

Nilizaliwa katika aila ya walalahoi. Baba yangu alikuwa mpagazi na mama yangu alikuwa dobi. Tuliishi katika nyumba ya msonge, iliyokuwa na shimo hapa na pale. Ulimwengu ulitucheka na dunia kututupa mbali. Changamoto za maisha yalitukumba lakini hatukufa moyo. Tulifahamu kuwa maisha ni kama bahari. Sio maisha yawe

shwari nyakati zote. Kwa hivyo wazazi wangu walijifunga nira kwa chochote walichofanya.

Naam, asiye na wake ana Mungu. Sikuwa tajiri wa mali lakini Mola alikuwa amenitunukia ubongo. Shuleni nilikuwa wembe. Hakuna muhula niliokuwa nambari nyingine ila ya kwanza. Wanafunzi wenzangu walinitemea mate na kunidharau. Hata nilipowasaidia masomoni waliendelea kunicheka au kunibeza. Ikhlasi asante ya punda ni mateke. Kinyume na wao, nilikuwa mnyenyekevu na mwenye tabia njema kwa kuwa nilifahamu kuwa tabia nzuri ni kama dhahabu.

Nilipofika darasa la nane, kila mja alitarajia kuwa nitafaulu katika mtihani wa kitaifa. Nilijaribu kuonya wenzangu kuwa mzaha mzaha hutunga usaha lakini wakawa sikio la kufa lisilosikia dawa wala kafara. Walipokuwa wakichezea masomo, nilijizatiti ima fa ima masomoni, huku nikijua kuwa wahenga hawakunena waliposema kuwa mgaagaa na upwa hali wali mkavu.

Matokeo ya mtihani yalipotoka, nilikuwa nambari ya kwanza katika kijijini kote. Wazazi wangu nami tulifurahi kama mhangi aliyepata meno ya kula nyama. Sifa zangu zilienea kote kote kama moto mkasa wa kiangazi. Wengi walinipa mkono wa tahania, lakini

wengine walijawa na inda na inadi. Waama, bidii hulipa.

Nilijiunga na shule ya taifa nilipopata msamaria mwema aliyenisaidia kwa kulipa karo yangu. Nilipoona namna wazazi wangu walijifunga nira ili wanitunzi, nilijua kuwa lazima nisiwaaibishe kwa kufeli mtihani wangu wa kidato cha nne. Nikajifunga kisabuni masomoni.

Nipomaliza mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne, niliibuka kuwa wa kwanza katika nchi hii yetu ya Kasongora. Wazazi wangu walijawa na furaha ghaya. Niliitwa kujiunga na chuo kikuu, nikaamua kuwa daktari wa akili.

Sasa hivi nawaza kujitegemea na hata wengine kama wazazi wangu wananitegemea. Kweli, mchanikaye kwenye mpini hafi njaa."

Shangwe na nderemo zilisikika kote kote. Hakika nilikuja kuamini kwamba mtu akitia bidii katika jambo, hata liwe gumu vipi, hatimaye hufaulu.

Mtahiniwa huyu amedhihirisha kuwa ameielewa mada na kuiwasilisha kwa mtindo bora zaidi akilinganishwa na wa awali. Hata hivyo ubora wa insha yake umepujuliwa na makosa mengi ya sarufi, hijai, kimuundo na msamiati. Yafuatayo ni baadhi:

a) hotuba ya mgeni imeingizwa ghafla kwenye usimulizi
b) **shimo** badala ya **mashimo**
c) **changamoto yalitukumba** badala ya **changamoto zilitukumba**
d) **hitifaki** badala ya **itifaki**
e) **wanitunzi** badala ya **wanitunze**
d) amechopeka methali na msamiati mwingine, hivyo kuvuruga mtiririko na mshikamano wa mawazo.

Alama iliyotuzwa 29

**Kundi la Nne (Alama 31 – 40)**

Watahiniwa katika kundi hili kwa kawaida huwa wanaimudu lugha vizuri. Huwa na kiwango cha juu cha ubunifu kimaudhui na kifani. Hutumia lugha kwa wepesi kujieleza. Mijadala au masimulizi yao huwa na muundo bayana wenye mshikamano na mtiririko mzuri wa mawazo. Hawa huielewa mada na kuikuza kwa kiasi cha kuridhisha. Wale wanaotuzwa alama **31 - 35** huitumia lugha kwa wepes zaidi. Hata hivyo, insha zao huwa na makosa ya hapa na pale ya sarufi, hijai na msamiati.

Wale wanaotuzwa alama **36 - 40** huwa na umilisi wa lugha wa kiwango cha juu zaidi na huwasilisha mawazo yao kwa mitindo mbalimbali ya usimulizi au mitindo mbalimbali ya kujieleza ambayo huzipa kazi zao mvuto wa hali ya juu. Huteua msamiati unaoafiki mada na kuutumia vyema kufanikisha usimulizi au mjadala wao. Insha zao huwa na makosa machache mno ya sarufi, hijai na msamiati. Hali kadhalika hati zao zinasomeka kwa urahisi na wanatosheleza urefu.

**Mtungo wa Saba**

KINOLEWACHO HUPATA

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:

Hakika nilikuja kuamini kwamba mtu akitia bidii katika jambo, hata liwe gumu vipi, hatimaye hufaulu.

Janga lilikuwa limeikumba dunia yetu; ukongo wa Kahiki. Ulikuwa ukongo ulioshambulia insi na kuwaacha magofu ya watu. Ulikuwa wa kuambukiza na ulisambazwa kwa mwia mfupi. Iwapo adinasi angeathiriwa na ukongo huu basi kile ambacho kingesalia ni kifo chake.

Tayari waja ayami walikuwa wameenda kuzimuni, basi matarajio ya kurejea mumu humu duniani. Hospitali zilijaa kwani waja walikuja kutafuta matibabu, kila mmoja akihofia kuisalimu amri. Walipong'amua kuwa ukongo huo hauna tiba, wangeatuka moyo. Watoto na wazazi wao walimomonyoka huku uchungu usiotajika wala kuelezeka ukiwazonga. Wengi waliendelea kuathirika huku uchumi za nchi ukididimia didi. Iwapo tiba isingepatikana basi wakaa wetu duniani ungeisha.

Masaibu haya yote yakatufanya sisi, tukiwa matabibu, kusumbuka mchana kutwa na usiku kucha. Lengo letu lilikuwa kupata tiba. Kadri tulivyoendelea ndivyo waja walipoteza matumaini. Shirika la kimataifa duniani lilikuwa limewateua matabibu bora duniani kutafuta tiba; mie

nilikuwa miongoni mwao. Tulichanga bia kwani tulimanya fika kuwa mkono mmoja hauchinji ng'ombe laili wa nahari, tukawa maabarani tukizichanganya kemikali ainati ili tuweze kupata tiba. Kila wakaa, tukaambulia pang'and

Hebu tafakari na utafakuri. Nyinyi ni matabibu bora duniani. Nyote mmekabidhiwa jukumu la kutengeneza tiba ya kuyaokoa maisha. Wakaa huo huo, waja wanakata roho, wodi zimejaa sisemi mochari zenye wafu. Halafu kila mnapojaribu kubuni tiba, mnaambuli patupu. Hisia zako zingekuwa chanya au hasi?

Hata hivyo, hatukukufa moyo kwani tulimaizi fika kuwa mgagaa na upwa hali wali mkavu. Tukakata shauri kutafuta uauni kutoka kwa waganga na waganguzi waliotibu kwa mitishamba. Tuliweza kupata sampuli za miti ambayo iliweza kutibu maradhi ayami. Tukarudi maabarani tukijua kuwa iwapo hatungefanikiwa raundi hiyo kusingekuwa na lolote jingine la kufanya. Tulitia bidii za duduvule atoboaye shajari kwani aali hupatikana kwa ghali. Tukakosa malepe ya gonezi kwa usiku ayami. Mlo nao hatukuwa na haja kubwa nao. Haja yetu ilikuwa kupata tiba.

Baada ya yaumu si kidigi, tulibuni dawa. Hatukuwa na uhakika kuwa tungefanikiwa. Ilikuwa jaribio letu la mwisho. Tulipata mja

ambaye angetiliwa dawa hiyo mwilini. Waja wote walikuwa macho. Tulimdunga sindano na kusubiri kwa siku tandatu. Wakaa huu wote wasiwasi wa mwasi ulitutawala. Tungefaulu? Ndilo lililokuwa swali kwenye taamuli zetu. Tuliriaria kama mtetea aliyekoso mahala pa kutaga.

Siku ilipowadia, tulichukua sampuli ya ngeu yake na kwenda maabarani kuiangalia. Moyo wangu ulidunda kama ngoma za mahepe tulipokuwa tukisubiri. Mja yule alionekana mwenye siha lakini hiyo haikuwa hakikisho la kuumaliza ukongo. Kadiri mwia ulivyoyoma ndivyo tulivyojawa na kihereherie.

Amini usiamini, tulikuwa tumeumaliza ukongo. Mwia wa nyuni kumeza punje, tulitangaza kuwa tulikuwa na tiba. Bishara na bashasha ilitutingo si kidogo. Tulichokosa ni mabawa kwani tungepaa angani. Baada ya kudhurika tulikuwa tumepata la waridi. Tiba ilipatikana. Hufyu! Hatari ilikuwa imeisha.

Hakika nilikuja kuamini kwamba mtu akitia bidii katika jambo, hata liwe gumu vipi, hatimaye hufaulu.

Mtahiniwa huyu ameielewa mada na kuikuza vyema na kwa ukomavu zaidi kimaudhui na kifani. Tofauti na watangulizi wake. Anatumia vipengele vya kimtindo kama vile usawiri wa mandhari na ulinganishaji kwa ufanifu bila kuvuruga muwala na muumano wa mawazo yake. Tofauti na watangulizi wake, anahisika zaidi kuwa anawasiliana na hadhira yake moja kwa moja. Mawazo yanatiririshwa kimantiki kiasi, hata hivyo mtahiniwa huyu ana makosa ya sarufi na hijai kama vile.

a) **ndivyo waja walipopoteza** badala ya **ndivyo waja walivyopoteza**
b) **tulibuni dawa**, badala ya **tuligundua dawa**
c) **hatukukufa** badala ya **hatukufa**
d) ange - fuswa
e) **walimamia**
f) **tunge fanikiwa** badala ya **tungefanikiwa**

Aidha mtahiniwa huyu anatumia msamiati wa kishairi kama vile **insi, adinasi**. Ana matumizi mabaya ya msamiati kama vile **ayami.**

Alama iliyotuzwa: **33**

**Mtungo wa Nane**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.**

*Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.*

Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:

Hakika nilikuja kuamini kwamba mtu akitia bidii katika jambo, hata liwe gumu vipi, hatimaye hufaulu.

ACHANIKAYE KWA MPINI HAFI NJAA

Uwanja uligonda kwa kimya cha maziarani. Dua lilikuwa karibu kutumwa kwa Mwenyezi Subhana wa Taala kumwomba azidi kuionekania nchi yetu. Azidi kunikarimu mimi, anitoshelezee matilaba yangu yote. Najua ungeuliza kwa nini mimi? Hata mimi mwenyewe sikusadifu haya yote yalikuwa yakitendewa kwangu mimi karimu mwana wa Hisani.

"... tunaomba tukiamini Amina." Kasisi alikamilisha maombi yake na nikaelekezwa kurejea kitini pangu. Macho yote yalikuwa kwangu huku shamrashamra, vikorombwe na makofi yakihinikiza hewani. Wengi hawakuamini kuwa mimi nilikuwa sasa mshindi wa tuzo ya dunia ya Nobeli kutokana na juhudi zangu za kutetea haki za wasichana na kuwa mstari wa mbele katika vita dhidi ya ukeketaji.

Niliabiri mashua ya mawazo na kuzama zii katika bahari ya fikra zangu. Nilikumbuka jinsi moto huu wa kuwatakia kila mwanajamii haki sawa ulivyoanza kurindima kwenye chembe cha moyo wangu. Baada ya kulazimishiwa ukeketaji nisingependa banati yeyote yule apitie dhuluma kama hiyo. Hayo

ni mateso - mateso yasiyokuwa na chuki. Ukiwanena hivyo wavyele hawasikii eti mwocha mila ni mtuma. Pukachaka!

Nakumbuka jinsi nilivyotembea nchini kote nikiwasihi waja waache tamaduni hii ya jadi na jadudi iliyopitwa na wakati! Nilianza na kuwaomba maswahiba wangu kuandamana nami katika mkondo huu niliokuwa nataka kuufuata. Swali langu hili lilakiwa kwa vicheko. Vicheko vya stihizai na kejeli eti zangu hizo zilikuwa ndoto tu! Nikapiga moyo konde. Haidhuru. Nilikuwa nimekwisha amua. Ningalijaribu kadri niwezavyo kubadilisha fikra za adinasi kuhusu suala hili.

Kutembea kwingi ndiko kuona mengi! Wazingapole waligonga ndipo. Hapo awali nilipozuru miji karibu na jiji kuu walikubali na kughairi tamaduni hii miongoni mwao. Hii ilinipa nguvu ya kujifunga kibwebwe katika kukurukakara zangu. Lakini sikujua kuwa yaliyonisubiri mbele yalikuwa ya zimwi lisilokujua ambalo mipango yake ni ya kukumaliza. Nilipofika kaskazini mwa nchi nilijua kuwa huku ndiko ukeketaji ulipoherehekewa kwa vifijo na shangwe. Basi nilipokuwa nikizungumza na akina mama wa eneo hilo nilitahadhari kwa mengi. Lakini hata machache niliyoyasema yalionekana kuwa kisu kilicholisengasenga maini yao na kuzua zogo na zahama. Mawa yaliokotwa na kulengwa

kwangu. Kosa langu nini? Ungejiuliza. Eti niliwakosea hadhi na staha. Nilipiga piyo nambari miguu niponye na kutorokea roho yangu.

Nilistaajabu ya Musa ningeyamudu ya Firauni? Wakati ulifika nilipokuwa natafaa kuzuru kwetu eneo la Songanyuma. Nililakiwa vizuri lakini pindi tu nilipoanza kuzungumza yaliyonileta huko mambo yakaenda tenge tahanani. Huko kwingine kulikuwa mawe lakini huku nilishikiwa vimangore, mikuki na hata panga na watu wa jamii yangu.

Lakini hata hivyo niliongeza bidii katika harakati zangu. Yaliyopita si ndwele tugange yajayo, wengine wangesema. Niliamua kuyasahau yote niliyotendewa. Sasa leo niko katika hafla hii. Hafla ya kusherekea bidii zangu za mcumeno ukerezao mbao dhidi ya viti hivyo. Walionikashifu leo hawana pa kuonyesha uso. Hakika nilikuja kuamini kwamba mtu akitia bidii katika jambo, hata liwe gumu vipi, hatimaye hufaulu.

Mtahiniwa huyu ameielewa mada na kuiwasilisha kwa lugha komavu akilinganishwa na wale wa kiwango cha chini. Insha yake imebainisha uasilia na ubunifu wa kiwango cha juu. Uteuzi wake wa mada, pamoja na fani unaupa utungo wake shani. Pamoja na kutumia lugha kwa wepesi mkuu, mtahiniwa huyu amezungumzia suala ibuka; haki za kibinadamu/unyanyasaji wa kijinsia.

Kisa kimetumia tamathali za usemi na mbinu nyingine za kimtindo kwa ufanifu mkuu. Ametumia mbinu rejeshi, anazungumza moja kwa moja na hadhira, hali ambayo inafupisha masafa ujumi baina yake na msomaji. Makosa ya kisarufi, hijai, msamiati na kimuundo ni kama vile:

a) **ungeuliza** - njeo imetumika vibaya
b) **tamaduni hii - utamaduni huu**
c) **mawa - mawe**
d) **lakini hata hivyo - lakini / hata hivyo**. Mtahiniwa hapaswi kuvitumia viunganishi hivi pamoja.
e) **kusherekea - kusherehekea**, nk.
f) **matokeo yalipotoka** badala ya **yalipotanganza/yalipotolewa**.

Alama iliyotuzwa: **35**

## 4.3 MAPENDEKEZO KWA WALIMU

4.3.1 Walimu wawahimize wanafunzi kufanya mazoezi zaidi katika mada tata za sarufi.

4.3.2 Ufunzaji wa msamiati uhusishwe na muktadha badala ya kuufunza ukiwa mkavu. Kwa mfano, msamiati wa magonjwa unaweza kufunzwa kwa kutumia ufahamu kuhusu magonjwa.Hili litamwezesha mwanafunzi kuuelewa msamiati katika matumizi halisi.

4.3.3 Wanafunzi wahimizwe kutumia ujuzi wa waliyosoma katika ufahamu kujibu maswali ya ufahamu badala ya kukariri au kuchopoa mawazo moja kwa moja kutoka kwenye vifungu.

4.3.4 Wanafunzi wahimizwe kutumia mbinu bora za kuukabili ufahamu. Badala ya kusoma swali, kisha kuanza kutafuta majibu, wasome ufahamu kwanza kabla ya kuyasoma maswali na majibu yaliyotolewa.

4.3.5 Walimu watunge maswali yanayopima stadi mbalimbali (ngazi/viwango) tofautitofauti za maarifa au utambuzi wala si stadi ya kukariri/ujuzi pekee. Hili litamzoesha mwanafunzi kujibu maswali ya aina tofautitofauti katika mtihani.

4.3.6 Stadi ya kusikiliza na kuzungumza ihimizwe zaidi kupitia utambaji, mijadala na imla, ili kuboresha maendelezo na kuimarisha mitindo ya kujieleza au mitindo ya usimulizi..

4.3.7 Wanafunzi wasisitiziwe umuhimu wa kusoma vitabu na makala mbalimbali ili kukuza ubunifu.

4.3.8 Wanafunzi waonywe dhidi ya kushinikiza msamiati usiohitajika katika insha. Hili hufifilisha mawasiliano na kuifisidi insha mvuto wake.Msamiati unaoteuliwa sharti uoane na mada na kuafikiana na msamiati au matini jirani katika sentensi ambamo umetumiwa.Msamiati wa kishairi usitumiwe kuandika tungo zisizo za kishairi.

4.3.9 Walimu warejelee vitabu mbalimbali vilivyopendekezwa, wasitumie kimoja tu.Hili litawapa wanafunzi uwanja mpana wa kujifunzia.

4.3.10 Walimu wawasisitizie wanafunzi umuhimu wa hati nzuri ili kurahisisha usomaji na usahihishaji wa insha zao na kuzipa kazi zao mvuto chanya.

4.3.11 Walimu wawahimize wanafunzi kutumia Kiswahili zaidi katika mazungumzo yao ili kuimarisha mikakati ya kujieleza na kusimulia kwa kwacho.

4.3.12 Walimu wawaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kufasiri mada/maswali mbalimbali ili kukinga dhidi ya kupotoka kimaudhui.

4.3.13 Walimu wawape wanafunzi mazoezi ya mitindo tofautitofauti ya insha ili wapate uzoefu wa kuandika aina mbalimbali za insha.

4.3.14 Walimu watumie mwelekeo mseto katika ufunzaji wa mada mbalimbali, kwa mfano mada changamano za kisarufi. Mathalan, mwalimu anaweza kutumia vitabu vya hadithi kufunzia dhana za kisarufi kama vile njeo, hali na aina za maneno. Hili litakinga dhidi ya wanafunzi kuziona dhana hizi kuwa dhahania. Itakuwa rahisi kuzielewa dhana hizi zikitokea katika matumizi halisi. Kadhalika hili litayafanya mafunzo ya sarufi kuwa ya kuvutia zaidi, hivyo wanafunzi watayachangamkia na kuyaelewa zaidi.